SURA YA PILI
KWA NINI NI MUHIMU KUWAFUNDISHA WATOTO?

Mara nyingi watu hufikiri kuwa wale ambao ni muhimu kweli " watu mashuhuri" ni wale wenye majina na vyeo. Tunafikiri ni wale wenye nafasi za madaraka kanisani. Wakati mwingine tunafikiri ni wale wafundishao watu wazima ndio wenye umuhimu zaidi.

Hii ni sababu ya kwanza itupasayo kuwafundisha watoto neno la mungu.

1. WATOTO NI MUHIMU NA WENYE THAMANI KUBWA KWA MUNGU

Tunajua kuwa watoto ni wenye thamani kubwa kwa Mungu, kwa sababu Yesu Kristo alitoa muda wake kuwabariki wao. Soma Mt.19:13-15. Je watu walitaka Yesu awafanyie nini watoto?

……
……

Fikiria hili:

Mawazo yao na hisia zao vilitokana na matendo yao. Waliwakataza wale waliotaka kuwaleta waatoto wao kwa Yesu. Pengine walifikiri kwamba Yesu alikuwa na kazi kubwa muhimu ya kufanya hivyo asingesumbuliwa nao. Lakini kama ndivyo, Yesu hakukubaliana na mawazo yao. Wanafunzi waliwakataza wazazi waliowaleta watoto kwa Yesu, lakini YEYE alipoona hilo, badala yake aliwakataza wao. Aliona kuwa mawazo yao yalikuwa maovu. Je ni mambo gani mawili Yesu alisema kuhusu watoto katika Mt. 19:14?

……
……..

Fikiria hili.

Kwanza Yesu aliwaamuru wasiwakataze watoto kuja kwake. Pili, lazima waondokane na kuwazuia au kuwakwaza au kusimama katika njia yao ya kuja kwa Yesu. Baada ya Yesu kusema haya, aliweka mikono yake juu yao na kuwabariki. Yesu alitoa muda wake bure kwa watoto. Pamoja na kuwa alikuwa na kazi nyingi muhimu ya kuwafundisha watu wazima, alitoa muda wake na nguvu kwa ajili ya watoto kwa sababu alifahamu umuhimu wao. Aliwapa wanafunzi wake mfano huu, na kuwaagiza kufuata mfano wake moja kwa moja. Fikiria mtazamo wako kuhusu watoto, Je mtazamo wako unaendana na Yesu anavyotaka na kufundisha? Andika hapa ni nini vinahitajika kubadilika katika mtazamo wako na matendo yako kuhusu watoto.

……
…….

Sasa omba msaada wa Mungu ili kubadili mtazamo na matendo haya. Andika maombi yako hapa:

……
……
……

2. WATOTO NI WENYE DHAMBI; HIVYO WANAHITAJI KUOKOLEWA

Mara nyingi tumefikiri kwamba watoto wako huru hawana dhambi. Hufikiri kuwa lazima Mungu atawachukua wote mbinguni. Je, hivi ni kweli kwamba watoto wako huru bila dhambi na wote wanaenda mbinguni?

Fikiria hili:
Umepata kumwona mtoto akitenda jambo baya, wakati akijua na kuelewa kuwa hilo ni baya? Ndiyo, nafikiri sote tumeona hilo. Ninafikiri sasa juu ya mazoea fulani tulikuwa nayo kutokana na mtoto wetu wa kwanza. Alikuwa na miaka mitano tu wakati huo.
Kila tulipoona amefanya jambo, tulimwita atueleze kwanini amefanya vile. Lakini kabla hata hatujamuuliza swali, alikimbia. Alijificha chini ya kitanda chake. Unadhani kwanini alikimbia?
……
……..
Fikiria hili.
Alikimbia kwa sababu alielewa vizuri kabisa kuwa alikuwa ametenda jambo baya.Ndiyo maana aliogopa. Licha ya kuwa alikuwa mtoto wa miaka mitano tu.

Mara nyingi, watoto huelewa kuwa wanafanya vibaya, lakini wao wenyewe huchagua njia mbaya. Siwezi kusema ni katika umri gani watoto huanza kutambua jema na baya na wao wakachagua baya huku wakielewa ni baya. Ni tofauti kwa kila mtu. Mtoto mwereve ambaye amepokea mafundisho mazuri anaweza kutambua jema kutoka baya akiwa na umri wa miaka 4 au 5. Baadhi ya watoto wanaweza kuelewa mapema zaidi ya muda huo. Wengine, ambao hijifunza polepole, au ambao hawakupata mafundisho mazuri, wanaweza kuwa na umri wa miaka 7 au 8 kabla ya kuanza kutambua jema toka baya. Baadhi ya watoto wamelemaa kiakili. Hawatapambanua jema toka baya, hata kama watakuwa watu wazima. Hakuna njia mtu yeyote anaweza kusema ni katika umri gani mtoto huwajibika mbele za Mungu, lakini Mungu mwenyewe anajua ni umri gani, hii ni kwa kila mtu.

Mtoto anapokuwa amefikia umri au kiwango cha kuelewa na kuatmbua jema na baya, mtoto huyo sasa huwajibika mbele za Mungu na kwa Mungu. Kama akielewa kuwa jambo fulani ni baya, naye akachagua kulifanya hivyo hivyo, atakuwa ametenda dhambi machoni pa Mungu na Mungu atamwajibisha kwa dhambi yake, ingawa ni mtoto mdogo. Soma Rum. 3:23. Je ni watu wangapi wametenda dhambi? Hali hii inakuwaje kwa watoto?
……
…….
Fikiria hili.
Kila mmoja ametenda dhambi……kila mmoja. Ni hakika watoto nao wamejumuishwa katika nenon hili “wote.“ Watoto pia wametenda dhambi. Soma Rum.6.23. Dhambi zetu zimeleta nini kwetu?
……
……
Fikiria hili.
Dhambi imetuletea mauti ya kiroho. Kwa vile watoto nao wametenda dhambi, wao nao wana tatizo hili la mauti ya kiroho.Kama watoto wamechagua kufanya baya, na wameelewa kuwa lile walilochagua ni baya, basi wamefanya dhambi, na wanahitaji kuokolewa, kama vile watu wazima. Soma Mt.18.14. Yesu alisema, “Vivyo hivyo haipendezi mbele za baba yenu aliye mbinguni kwamba mmoja wa wadogohawa wapotee“ Je tunajuaje kuwa inawezekana kwa watoto kupotea?
……
……

Fikiria hili.
Kwa kuwa Mungu amesema hapendi mtoto mdogo apotee, hii inaonesha kuwa INAWEZEKANA kwa mmoja kupotea. Inawezekana. Wanaweza kupotea, lakini Mungu hapendi itokee hivyo. Soma Mt. 18:10-13. Kabla Yesu hajasimulia mfano wa kondoo aliyepotea, Yesu alikuwa akizungumza juu ya nini?
…….
Jibu:
Alikuwa akizungumza kuhusu watoto. Kondoo aliyepotea katika mfano ule ilimaanisha kuwa ni MTOTO. Mara mtoto akikua kidogo, mapema huanza kuanguka dhambini, kwa sababu ana moyo utendao dhambi, kama walivyo watu wazima. Kama mtoto ameanza kuchagua yale ajuayo ni mabaya, basi sasa anawajibika mbele za Mungu.

Matendo yetu wenyewe yanaonesha ukweli huu, vivyo hivyo matendo ya watoto wetu pia. Kama mtoto mchanga wa siku tatu akilia hatumtupi. Hatumpi adhabu, kwa sababu hajui afanyalo. Hafahamu lililo jema kutoka katika ovu., Lakini kama mtoto wa miaka mitatu akilia bila sababu inawezekana kwa wazazi wake kumwadhibu. Kama mtoto wa miaka kumi na minane akiendekeza kulia tunaweza kabisa kumwadhibu vikali kwa sababu anajua kuwa analia kwa kusudi la kutaka kufanikiwa mambo yake. Mungu ni mwenye haki. Watoto ambao hawajui kitu chochote tutawaacha watoto wale mikononi mwa Mungu. Lakini lazima tufahamu kuwa mara nyingi watoto huwa wanafahamu yale wayatendayo. Wanaelewa vizuri kuwa wanafanya dhambi, lakini wanataka mambo yao na wanafanya.

Je unafikirije? Kama mtoto yule akifariki dunia ataenda wapi? Hakuna njia itakayomwezesha kuingia mbinguni kama amefanya dhambi. Biblia inasema kuwa kuna mahali pawili tu mtu anaweza kwenda akiisha kufariki. Kuna mbinguni, Mungu akaapo. Kuna jehanam, ziwa la moto, ambapo shetani ataishi wakati fulani milele. Kama mtoto kwa hiari yake na uelewa wake amechagua dhambi, anahitaji wokovu upatikanao katika Yesu Kristo. Iwapo hampokei Yesu moyoni mwake na maishani mwake, hakuna njia itakayomwezesha kwenda mbinguni.

4. WATOTO WANAWEZA KUMTUMIKIA YESU KATIKA UTOTO WAO NA MAISHA YAO YOTE

Sababu ya nne kuwa tunawafundisha watoto ni hii: Kama watoto wakimpokea Yesu utotoni, wanaweza basi kuanza kumtumikia Yesu wangali watoto, na kuendelea kumtumikia Yeye maishani mwao mwote.

Sio watu wazima tu waweza kulitumikia kanisa, Sio watu wazima tu waweza kuwaongoza wengine kwa Yesu. Sio watu wazima tu waweza kuomba na kupokea majibu ya maombi yao. Si watu wazima tu wawezao kumuenzi Yesu katika maisha yao ya kila siku. Waamini wa kila umri wanaweza kufanya haya. Watoto pia wanaweza kumtumikiaYesu katika utoto wao.

Je, unawakumbuka baadhi nya watoto katika Biblia ambao walilisaidia kanisa? Soma Mdo. 12. Utaona habari ya msichana aliyeitwa Rhoda. Aliomba kwa ajili ya Mtume Petro pamoja na watu wazima. Nafikiri itakuwa ni imani ya Rhoda iliyomtoa Petro gerezani, kwa sababu hakuna miongoni mwa watu wazima wale aliyeamini Mungu alipojibu maombi yao. Ni Rhoda peke yake aliyeamini.

Maombi na imani ya msichana mdogo huyu yalilisaidia kanisa. Kama Petro angefia gerezani, tusingekuwa na vitabu vfya Waraka wa Kwanza na Waraka wa Pili wa Petro katika Biblia zetu leo. Vitabu hivi kwa namna moja ni vipawa ambavyo msichana huyu Rhoda alilipatia kanisa. Kweli msichana huyu mdogo aliokoa maisha ya Mtume Petro kwa maombi yake na imani yake.

Je, waweza kufikiri moja ya njia ambayo watoto wanaweza kulisaidia kanisa?
……
……

Fikiria hili:
Watoto wanaweza kulisaidia kanisa kwa maombi yao, kwa sababu wana imani kubwa. Katika Mdo. 23. unaweza kuona tena jinsi kijana mdogo alivyoyaokoa maisha ya Mtume Paulo. Tusingekuwa na vitabu 12 au 13 vimeandikwa na Mtume Paulo kama kijana huyu asingelitumikia kanisa.
Je, kijana huyu alifanyaje?
……
……

Jibu:
Kijana huyu aliwaambia wenye mamlaka kuwa baadhi ya watu wamepanga njama ya kumuua Paulo. Ujasiri wake wa kusema kwa wazee uliokoa maisha ya Paulo.

Andrea alipokuja kwa Yesu, kitu kingine alichofanya kilikuwa ni kumleta ndugu yake mkubwa kwa Yesu (Soma Yn. 1:41). Nimeona kuwa mara nyingi, mtoto anapokuwa amempokea Yesu jamaa lake wanapoona badiliko kubwa linapotokea kwa mtoto wao, nao hutaka kumpokea Bwana. Mtoto anaweza kuliongoza jamaa lake lote kwa Yesu. Je, unajua jamaa lililokuja kwa Yesu kwa sababu mtoto wao alimpokea Yesu kwanza? Ni nani?
……
…….

Je, uliandika jina la nani? Mara kadhaa watoto wameongoza jamaa zao kwa Yesu. Huko Marekani msichana mdogo alimwomba babake kuja Shule ya Jumapili pamoja naye. Babake hakuwa mtu wa imani. Hakuwa na shauku na mambo ya Mungu. Alimwahidi bintiye kuwa atakuja tu kwa kuwa ameendelea kumsihi, lakini akasema ukweli ni kuwa hataingia kanisani. Ataingiza mguu mmoja tu mlangoni. Alipofika kanisani, yule msichana mdogo aliuvuta kwa nguvu mkono wa babake, na akamvutia babake ndani kanisani. Alikaa na akasikia Injili. Alimpokea Yesu kuwa mwokozi wake. Baada ya hapo baba alipenda kuja kanisani. Alienda mbali kusaidia vijiji vingi kuanzisha Shule za Jumapili. Yeye mwenyewe alianzisha Shule za Jumapili 1300 nchini Marekani, ilipokuwa ikingali changa na isiyoendelea. Aliwaongoza maelfu kwa Yesu. Tazama jinsi yule msichana mdogo alivyolitumikia kanisa.
Je, ni kwa njia ipi nyingine watoto wanaweza kulitumikia kanisa?
……
…….

Watoto wanaweza kutoa maisha yao yote kwa Mungu, na wanaweza hilo tu. Watu wazima hawana tena maisha yao yote. Tayari wameshatumia sehemu ya maisha yao. Tafakari Rumi 12:1. Mtume Paulo aliwasihi ndugu waaminio kuitoa miili yao kwa Mungu. Lakini hebu fikiria hili: Kama mtu Fulani akija kwa Bwana akiwa na umri wa miaka 60, je ni miaka mingapi ya upendo na utumishi atakayotoa kwa Mungu? Hata akija akiwa na umri wa miaka 30, bado atakuwa amepoteza miaka mingi dhambini. Mungu anawataka ndugu waaminio wote kutoa miili yao kwake, ni kweli, lakini WATOTO TU ndio wawezao kutoa maisha yao yote. Kila mmoja anaweza kumpa Mungu sehemu ya maisha yake, haijalishi amebakiza kiasi gani- lakini ni watoto tu wawezao kutoa maisha yao yote kwake. Je, ni nani awezaye kumpa Mungu zawadi kubwa basi, mtu mzima mwenye miaka 40 labda au mtoto wa miaka 8? Je, unaonaje?

……
……

Jibu:
Nadhani mtoto anaweza kumpa Mungu zawadi kubwa zauidi kwa sababu anaweza kumpa maisha yake yote. Anaweza kumtumikia Mungu sasa utotoni na baadaye katika utu uzima.

Je, umepata kumwona mtoto hapa Afrika aliyemtumikia Yesu na kanisa lake kikamilifu? Je, ni nani na ulionaje?

Kama hujaona hili sasa fumbua macho yako wazi. Nafikiri siku chache zijajo utaona watoto wengi wakimtumikia Mungu kwa ukamilifu. Hata hivyo tusipoona sana hilo, huenda inaonesha kuwa tumekuwa hatuwafundishi Neno la Mungu. Ni budi tuanze kuwafundisha na kuwaongoza wao kwa Yesu. Kisha watape kujiamini na kuanza kumtumikia Yesu.

5. WATOTO NI KANISA, TAIFA NA WAZAZI WA KESHO.

Ni watoto leo, lakini hawatabaki watoto kwa muda mrefu. Muda si mrefu watakuwa vijana, watu wazima na viongozi wa makanisa yetu na jumuiya . Watakuwa wazazi. Watakuwa viongozi wa serkali zetu siku zijazo. Mtu yeyote atakayekuwa kiongozi katika miaka 20 au 30 ijayo ni mtoto kwa sasa. Leo wewe na walimu wengine wa watoto mna nafasi ya kumfundisha na kumwongoza katika njia ifaayo, ili kwamba baadaye atakuwa raia mwema na pengine kiongozi bora. Unaweza ukawa unamfundisha mchungaji wa siku zijazo, kiongozi wa kanisa, kiongozi wa kijiji au kiongozi wa familia. Fikiria wale wanaoongoza kanisa na nchi leo. Andika majina yao hapa.

……
……
……
……

Je umeandika majina ya viongozi wa sasa? Ni wazi kuwa watu hawa wote kwanza walikuwa watoto. Nani watakuwa viongozi wa kanisa na taifa lako siku zijazo? Hatujui, lakini twafahamu kuwa kwa sasa bado ni watoto wadogo; ama hawajazaliwa bado nao watakuwa watoto miaka ijayo. Kama kanisa likiwafundisha watoto Neno la Mungu, litakuwa likiwafundisha na kuwaandaa viongozi wa kesho pia.

Iwapo hatuwafundishi watoto Neno kla Mungu, ni budi tufahamu kuwa wakati sisi watu wazima tutakapokufa ukristo utakufa pamoja nasi. Imani katika Yesu haitabaki ulimwenguni.Watoto hawataendelea tena kumkiri Yesu kama Bwana wao. Je tutawezaje kupata uhakika kuwa siku zijazo watu wataendelea kumfuata mwokozi? Isipokuwa tu tutakapowafundisha watoto wetu Neno la Mungu leo.

Bila shaka unajua kidogo historia ya nchi yako. Je unajua baadhi ya vijiji ambavyo zamani vilikuwa imara katika Neno la Mungu na sasa sio hivyo? Andika uchunguzi wako hapa:
……
……..

Fikiria hili:
Iwapo baadhi ya vijij vilikuwa imara katika imani na sasa sio hivyo, ni dhahiri wazazi na viongozi wa kanisa hawakufanya kazi kamilifu ya kuwafundisha watoto wao Neno la Mungu. Hali hii ilitokea kwa Wayahudi pia. Yoshua alikuwa kiongozi mzuri na imara. Soma Yos. 24:24. Chini ya uongozi wake, je ni ahadi gani waliyotoa kwa Mungu?
……
……
Jibu:
Waliahidi kumfuata Mungu, na walifanya hivyo siku zote za maisha ya Yoshua. Wakuu nao pia walimfuata Mungu maishani mwao mwote. Lakini baadaye kitu kibaya cha kuhuzunisha kikatokea! Hawakuwa wamewaongoza watoto wao katika njia za Mungu. Soma ilivyotokea katika Waamuzi 2:12-13. Walipokuwa wamekufa, watoto wao walipotoka kutoka njia za Mungu na kutengeneza na kutumikia sanamu. Mungu alighadhabika kwa uovu waliokuwa wametenda, hivyo akailaani nchi yao. Oh! ni huzuni gani hii, na yote hayo kwa sababu hawakuwaongoza watoto wao katika njia za Mungu

Baada ya miaka 20, je viongozi wa kanisa watakuwaje? Baada ya miaka 30 je? Baada ya miaka 50 je? Kwa kiasi kikubwa ustawi wa kanisa utakuwa mikononi mwetu leo. Ni sisi tunaopaswa kuwafundisha watoto ambao watakuwa viongozi wa kanisa nyakati zijazo. Twatambua kuwa kama mtu fulani hakuzaliwa kwa Roho wa Mungu, hawezi kufahamu ukweli wa kiroho. Hata kama atahudhuria ibada za sifa pamoja nao waaminio, hata kama atazungumza kama aaminiye, hata kama atakuwa amepitia ubatizo au kushiriki ushirika mtakatifu, kama atakuwa hajazaliwa kwa Roho wa Mungu, hataweza kutafuta vitu vya kiroho, hatafahamu vitu vya kiroho, hatavitamani vitu hivyo. Soma I Kor.2:14. Je, inasemaje kuhusu mtu asiye na Roho wa Mungu?
……
……..

Jibu:
Mstari huu watuambia kuwa mtu asiyekuwa na roho wa Mungu hawezi kupokea au kuyatambua mambo ya rohoni. Hawezi kuyafahamu mambo ya rohoni, kwa sababu mambo haya hutoka kwa Mungu naye hana Roho wa Mungu ndani yake. Hufikiri mambo ya Mungu ni upuuzi. Je, tutafahamuje umuhimu wake?

……
……

Fikiria hili:
Hakuna njia, watakuwa waaminio wa kweli iwapo watatubia dhambi zao na kuweka imani yao katika Yesu Kristo. Bila hivyo, mambo yote haya mengine hayawezi kumpendeza Mungu. Soma Rum. 8:9. Je, mtu humpokeaje Roho wa Mungu?

Jibu:
Mungu humpa mtu Roho wake pale anapotubia dhambi na kumwamini Yesu Kristo kuwa Mwokozi na Bwana wake. Waaminio wote wana Roho wa Mungu lakini si kila mtu awaye yote anaye. Watoto pia wanaweza kufahamu ukweli wa rohoni iwapo tu wataweka imani yao kwa Yesu. Iwapo baadaye watakuwa viongozi na wakuu katika kanisa, kisha wakawa hawakumjua Yesu mioyoni mwao, watafuata tamaa zao za asili. Kama viongozi wa kanisa mawazo yao na tamaa zao vitajikita katika kujineemesha na kujiendeleza wenyewe. Uongo, wivu, na kiburi haya yote yatainuka kanisani bila kizuizi. Je, tutafanyaje kuhakikisha haya hayatokei hivyo?
……
…….

Hebu fikiria hili:
Nadhani tunaweza kusaidia kuzuia hili lisitokee kwa kuwafundisha watoto Neno la Mungu, na kuwaongoza kuweka imani yao kwa Yesu. Kwa njia hiyo watakuwa wakristo si katika utumishi wao tu bali mioyoni. Sionei shaka wao kuwa wakristo tu, bali kuhesabiwa na Mungu mwenyewe kuwa waaminio wa kweli. Tukiwafundisha watoto wetu Neno la Mungu na kuwaongoza kwa Yesu, watafuata mambo ya Roho. Watafahamu mafundisho ya Biblia, hivyo watakuwa viongozi bora wakati fulani wataliongoza kanisa vyema. Soma Rum.10:1. Kabla watotio hawajamwabudu Mungu wanapaswa kufanya nini kwanza?
……
……
……..
Jibu:
Kabla mtu awaye yote hajamwabudu Mungu, anapaswa kumwamini Yeye. Rum. 10:14. inauliza, : “Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini?” Kabla watoto hawajamwamini Yesu, sisi viongozi tunapaswa kufanyaje?
……
……..

Jibu:
Tunapaswa kulifundisha na kulihubiri Neno la Mungu kusudi watoto wapate kulisikia na kulielewa. Kama tukitaka watu waweke imani yao kwa Yesu, ni budi kwanza tuwafundishe Neno la Mungu. Tukitaka viongozi wa siku zijazo wamjue Yesu ni lazima tuwafundishe leo. Iwapo tunataka viongozi wa siku za usoni kufuata kweli ya kiroho, ni

budi tuwafundishe kweli toka Neno la Mungu sasa, wakati huu wawezao kuja kwa Yesu kwa urahisi.

6. MUNGU AMETUAMURU KUWAFUNDISHA WATOTO WETU.
Tunapaswa kutii amri yake. Tangu zamani za Agano la Kale, Mungu amewaonesha watu wake kuwa wanapaswa kuwafundisha watoto wao.Soma Kumb. 6:2,6 na 7. na mistari 20-25. Fikiria hasa mstari wa 7. Mungu alituambia tuwe WENYE BIDII kuwafundisha watoto wetu na kwamba tuwajibike WAKATI WOTE, tukitumia kila nafasi atupayo. Je, mistari hii inafundisha kuwa tuwafundishe kidogo tu? Unaelewaje mistari hii?
……
……

Jibu:
Mungu ametuamuru kuwa imetupasa kuwa wenye bidii katika kuwafundisha watoto wetu. asubuhi, mchana ana usiku. Muda wote. Ni lazima tufanye bidii kuwafundisha. Kama pasingekuwa na sababu nyingine kabisa ya kuwafundisha watoto wetu, kwa hakika amri ya Nungu ingetosha kuwa sababu. Mungu ametuambia na kutuamuru kuwafundisha wao. Tunamwita Mungu “ Bwana wetu” hivyo tunapaswa kuwa tayari kutii amri zake

7. KANISA LA AWALI LILIWEKA MFANO KWETU WA KUWAONGOZA WATOTO KWA YESU
Soma Efeso 6: 4. Mtume Paulo aliandika barua hii kwa waaminio wa mji wa Efeso. Je Paulo alisemaje kuhusu wazazi wanavyopaswa kuwafundisha watoto wao?
……
……

Jibu:
Paulo alisema wanapaswa wawafundishe jinsi ya kuishi kama wakristo. Je malezi na maonyo ya Bwana inamaanisha nini?

Fikiria hili:
Malezi ya Bwana humaanisha jinsi ya kuishi kama waaminio. Inawaonesha waaminio nini wanapaswa kufanya ili kumpendeza Mungu na ni dhambi zipi wanapaswa kuziepuka. Mtume Paulo hapa anawaambia wazazi wawafunze watoto wao kama waaminio. Hii inaweza kuchukuliwa kuwa watoto tayari walishakuwa waaminio katika Kristo. Tafakari I Kor. 2:14. Iwapo watoto walikuwa hawajampokea Yesu, wangeelewaje mafundisho haya?
……
……..

Jibu
Wanaweza tu kuelewa vitu vya rohoni kama ni waaminio. Wale wasiokuwa na Roho wa Mungu hawawezi kufahamu mafundisho ya kiroho. Wanafikiri kuwa mafundisho haya ni upuuzi. Paulo anawafundisha wazazi kuwafunza watoto wao juu ya vitu vya Bwana. Hivyo, Paulo anadhani kuwa watoto wanaweza kufahamu mafundisho ya kiroho.

Anathibitisha waziwazi wanapaswa kuwa waaminio tayari. Wengie tayari waliisha waongoza watotowao kwa Yesu. Pengine walikuwa ni wazazi hawa hawa ambao walikuwa wamewaongoza watoto wao kwa Yesu. Watoto hawa lazima waliishakuwa tayari waaminio. Hivyo Paulo aliwaambia wazazi kuwafundisha vitu vya Mungu, ili wajue kumpendeza Mungu. Watoto wengi kanisani waliishakuwa waaminio tayari. Soma Efeso 6:1, Je Paulo anazungumza na watoto ndani kanisani au nje?

……
…….

Jibu:
Anasema kuwa watoto hawa walikuwa ndani ya kanisa, kwamba tayari waliishakuwa waaminio. Sasa soma Efeso 1:1. Angalia kuwa Paulo anaandika kitabu cha Waefeso kwa watu ambao ni waaminio. Anawatambulisha kama watakatifu au watu wa Mungu waliotengwa.

Soma Tit. 1:6.
Iwapo kanisa lilitaka kumchagua mzee wa kanisa liliangalia hali za watoto wake. Je, watoto wake walipaswa kuwaje?

……
…….
Jibu:
Watoto wa mzee wa kanisa lazima kwanza wawe waaminio. Pili, lazima wawe wapole na watiifu. Kama Paulo anaweza kutoa sheria kama hii kwa makanisa, inaonesha kuwa wengi wa waaminio walikuwa wakiwaongoza au tayari walikuwa wamewaongoza watoto wao kwa Yesu. Kanisa la mwanzo lilitupa sisi mfano mzuri katika jambo hili. Tunapaswa kuwaongoza watoto wetu kwa Yesu pia kama vile walivyofanya wale.

8. WALE WAWAONGOZA WATOTO KWA YESU WATAPOKEA THAWABU MAALUM TOKA KWA MUNGU BALI WAO WAWAPOTOSHAO KWA MUNGU WATAADHIBIWA VIKALI
Soma Luk. 9:46-48
Yesu alisema kuwa kama tukimpokea mtoto mdogo kwa jina lake, ni kama vile tulimpokea Yesu mwenyewe. Yesu alitutaka tujue kuwa watoto ni muhimu sana. Yesu alilinganisha umuhimu wa watoto wadogo na umuhimu wake mwenyewe. Tukimpokea mtoto mmoja mdogo katika Shule ya Jumapili, Yesu anasema ni kama tulimpokea Yeye mwenyewe, kwa sababu tunampokea mtoto kwa njia hii, tunafanya hivyo kwa upendo wake.

Wanafunzi wa Yesu walihojiana swali hili. “Ni nani atakayekuwa mkubwa miongoni mwao?” Yesu alijibu hivi: yule aliye mkubwa ni yule awatumikiaye hata watoto wadogo. Mungu ameahidi thawabu kubwa kwa wale wawafundishao watoto, lakini pia adhabu kubwa kwa wale wawapotoshao watoto. Soma Mt. 10:42. Je, Mungu ameahidi thawabu kwa nani katika mstari huu?

……
…….

Jibu:
Ameahidi thawabu kwa wote watoao walau kikombe cha maji baridi kwa mwanafunzi ambaye huonekana kama asiye na umuhimu wowote ule. Kikombe cha maji baridi ni kitu kidogo sana ambacho mtu yeyote angeona hakina umuhimu wowote. Pengine unawafundisha watoto na wengine hufikiri kuwa kazi yako sio ya muhimu sana. Wanachukulia kuwa ni kitu kidogo sana. Lakini hebu fikiria hili! Mungu huona ni kazi kubwa sana na muhimu. Unawapa watoto sio kikombe cha maji baridi ya kiu yao ya kimwili, bali maji ya uzima, maji ya roho. Je, ni kipi bora, watu waionavyo kazi yako au Mungu aionavyo kazi yako?

Fikiria hili:
Kipimo cha Mungu ni MUHIMU SANA, lakini watu hudhani ni chenye madhara kidogo tu.

Je, Mungu atatupa thawabu gani sisi tunaomtumikiaYesu? Ninaweza kuona aina tatu za thawabu katika Biblia kwa urahisi tu. Aina ya kwanza ya thawabu nionayo ni taji ambayo Mungu atatupa. Biblia inasema kuwa waaminio wataweza kupokea taji kwa jinsi walivyomtumikia Yesu. Tafakari I Kor.9:25, Ipet.5:4. na Ufu.2:110. Je unasoma kuhusu taji gani?
……
……
……..
Je, tutafanyaje na taji hizi? Je Mungu atatupatia sisi ili tuheshimiwe wenyewe? Oh! Hapana! Biblia inasema kuwa sote tutatupa taji zetu miguuni pa Yesu. Ona Ufu.4:10. Je unafikiri ni kwa nini tutafanya hivyo?
……
…….
Nadhani tutazitupa taji zetu miguuni pake kwa sababu tutampenda Yeye mno na hivyo tutataka kumheshimu Yeye kwa kutuokoa sisi. Lakini nilisema ninaona aina tatu za thawabu katika Biblia. Aina moja ni taji Yesu atakazotupa, taji ambazo tutatupa miguuni pake kumheshimu Yeye. Thawabu nyingine ni waaminio wenyewe tuliowaongoza kwa Yesu. Mtume Paulo aliwaambia wale aliowaongoza kwa Yesu kuwa watakuwa kama taji ya furaha kwake. (Fil. 4:1). Wao wenyewe walikuwa thawabu yake. Ufikapo mbinguni na kuwaona wale uliowaongoza kwa Yesu, je, hiyo haitakupa wewe furaha kubwa?
……
……

Ninaamini hiyo itamfanya kila aaminiye afurahi. Labda mtu fulani atakuja kwako huko mbinguni na kusema kitu kama hiki:
” Ndugu mpendwa, Ahsante, nilikuwa nikikiendea kifo, lakini nipo hapa mbinguni leo kwa sababu uliniongoza kwa Yesu”. Kama watu wengine watakuambia wapo hapo mbinguni kwa sababu ya mafundisho yako, je, hiyo haitakuwa thawabu ya ajabu?
……
…….

Kwangu mimi, nadhani hiyo itakuwa thawabu ya kuheshimika sana. Hivyo basi, thawabu moja ni taji za kutupa miguuni pa Yesu na nyingine ni furaha ya kuwaona wale ambao maisha yao yamebadilishwa kupitia huduma yako. Thawabu nyingine itakuwa ni kumsikia Yesu mwenyewe akisema, “Hongera mtumishi wangu mwema na mwaminifu.” Tutakaposikia hivyo, haitajalisha tena kama hakuna mtu au mtu aliyefikiri kazi yetu ilikuwa na umuhimu. Jambo muhimu basi litakuwa kujua kuwa Yesu aliikubali. Je, itakuwa thawabu kubwa namna gani kumsikia Yesu akisema, “Hongera.” Tutafurahi kiasi gani tukimsikia Yeye akituita sisi, “Watumishi wake wema na waaminifu.” Je, wadhani kuwa kukubaliwa na Yesu itakuwa ndiyo thawabu pekee utakayopokea kwa ufundishaji wako?

1. HEBU TUPITIE TENA:
Kamilisha kila kauli kurejea umuhimu wa watoto.

1. Kwa sababu wana……..
2. Kwa sababu wana…….
3. Kwa sababu wana……
4. Kwa sababu wana……
5. Kwa sababu wana……..
6. Kwa sababu Mungu……..
7. Kwa sababu kanisa la mwanzo……
8. Kwa sababu Mungu atatoa……

2. HEBU TUFANYE KWA MATENDO
Nimejitahidi kueleza sababu kadhaa kwanini ni muhimu kuwafundisha watoto Neno la Mungu. Sasa ninataka kukuuliza, Je, utajitoa kwa moyo kuwafundisha watoto? Je utaanzia walau kuwafundisha wanao au wale wa jirani zako na jamaa? Kama kanisa litatambua kuwa Mungu amekupa kipawa cha kuwafundisha watoto kanisani, je utakubali pia kuwa mwalimu wa Shule ya Jumapili? Tafakari kwa makini, kwa sababu hutakuwa unaniahidi mimi, bali Mungu.
ANDIKA AHADI YAKO MAHSUSI KWA MUNGU KUHUSU UFUNDISHAJI WA WATOTO.

Ninamwahidi Mungu kuwa …….
……
……
……
……
……
……
……
……
..